JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

Juni, 2023

Dodoma

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**


**Namba za Simu 0765842864**

**Mkuu wa Shule 0765842864**

**Makamu Mkuu wa Shule 0765960354**

**Patron 0757608048**

**Shule ya Sekondari KANTALAMBA**

**S.L.P. 70**


**Tarehe ..............................**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ............**
**...............................................**
**S.L.P ............................................**
**...............................................**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KANTALAMBA HALMASHAURI YA MANISPA YA SUMBAWANGA, MKOA WA RUKWA MWAKA 2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 Ninachukua nafasi hii kukupongeza kwa jitihada zako zilizowezesha kustahili uchaguzi huu. Nitegemeo langu kwamba jitihada hizo utaziongeza uwapo katika shule hii. Shule ina jumla ya michepuo minne ambayo ni HKL, HGK, HGL na EGM.

Shule ya Sekodari Kantalamba ipo katika Manispaa ya Sumbawanga. Manispaa hii ambayo ni makao Makuu ya mkoa wa Rukwa ipo umbali wa kilometa 336 toka Mbeya na kilometa 240 toka Mpanda. Upo usafiri wa uhakika kila siku toka Mbeya ambapo mabasi huondoka kuanzia saa 12:30 alfajiri na kuwasili Sumbawanga saa 7:00 mchana. Kutoka Mpanda usafiri upo kila siku ambapo gari huondoka saa 1:00 asubuhi na kuwasili Sumbawanga saa 7:00 mchana, shule ipo umbali wa kilometa tatu (3). Kwa kutumia usafiri wa tax utalipa shs.5,000/= na kwa kutumia bajaji utalipa shs. 1500/=. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza .................... unatakiwa kuripoti shuleni tarehe ..........................na mwisho wa kuripoti ni tarehe........................

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. **SURUALI 1 DARK BLUE**: Yenye malinda mawili kila upande na mkunjo au pindo chini (tumup) na isiyobana.

ii. **SURUALI 1 KAKI:** Yenye malinda mawili kila upande na mkunjo au pindo chini (tumup) na isiobana.

iii. **SURUALI 1 NYEUSI (YAKUSHINDIA):** Yenye malinda mawili kila upande na mkunjo au pindo chini (tumup) na isobana..

iv. **TAI 2**: Rangi dark blue na kaki (Suruali zote pamoja na tai zinapatikana shuleni)

v. **SHATI 2 ZA RANGI NYEUPE**: Mikono mirefu lenye mfuko mmoja kifuani upande wa kushoto.

vi. VIATU:
- Rangi nyeusi vyenye kamba, visiwe na soli nene, hairuhusiwi kuvaa viatu vya matairi,
- Kandambili au yeboyebo wakati wa masomo darasani na bwaloni/ukumbi wa chakula, haviruhusiwi.

vii. SOKSI:
- Rangi nyeusi isiyo na urembo wowote.

viii. MKANDA:
- Rangi nyeusi na uwe wa ngozi
- Usiwe na madoa au urembo wowote.

ix. T.SHIRTS:
- Rangi ya blue yenye kola.Tshirt zinapatikana shuleni zikiwa na nembo ya shule.
- Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na t-shirt 2.Kila t-shirt ni tshs 13,000/

x. **SWETA:** Rangi ya blue

xi. **NGUO ZA MICHEZO**

- Unatakiwa uje na nguo za michezo, bukta na fulana zote rangi ya bluu na track suit rangi nyeusi
- Uje na Raba kwa ajili ya michezo

**NB:** Hairuhusiwi kuja na nguo za nyumbani

## 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Uje na godoro futi 2½
ii. Chandarua na mashuka mawili ya rangi ya blue bahari
iii. Taulo, blanketi na Sanduku la chuma (original)
iv. Madaftari ya kutosha (counter books 7) na vitabu
v. copy ya cheti cha kuzaliwa
vi. Uje na results slip (original) na Leaving Certificate (Original)
vii. Uje na ndoo tatu za lita 10 kwa ajili ya (i) kuchotea maji ya jikoni (ii) kuchotea maji ya chooni (iii) na usafi binafsi
viii. Nguo za ndani za kutosha
ix. Nunua vyombo vya chakula ambavyo ni sahani, bakuli, kikombe pamoja na kijiko.
x. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
xi. Scientific Calculator (kwa tahasusi zinazohusu hesabu)
xii. Uje na mifagio 2 aina ya chelewa kwa ajli ya usafi wa mazingira
xiii. Uje na jembe lenye mpini.
xiv. Uje na drier 1 (Rubber squeezer/mopa)
xv. Uje na reki 1
xvi. Uje na fyekeo 1
xvii. Uje na brashi ya chooni.

## 2.3 Michango mbalimbali

### a) Shule za Bweni

| | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | Jumla | 80,000/= |

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi ,wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja**

**na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

**Saini ya Mkuu wa Shule** ..............................................

**Jina la Mkuu wa Shule** MUSA ALON MTAWA

**Mhuri wa Mkuu wa Shule** MKUU WA SHULE SHULE YA SEKONDARI KANTALAMBA S.L.P. 70 SUMBAWANGA

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.** TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- **Mkuu wa shule 0765842864**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0765960354**
- **Mwandamizi Taaluma 0786901495**
- **Mwandamizi Malezi 0757608048**

Fomu Na 1

SUMBAWANGA MUNICIPAL COUNCIL

KANTALAMBA SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 70,
SUMBAWANGA
DATE.............................................

MEDICAL OFFICER
GOVERNMENT HOSPITAL
...................................................
...................................................

REF: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A.

Name ..............................................................................................................................

Please examine the above named as to HIS/HER physical and mental fitness as indicate below and arrange for necessary treatment if required. This certificate must be signed by qualified medical officer of a government Hospital and returned to school by the student.

The examination should include the following categories:

1. Sight
2. Hearing
3. Haemoglobin
4. Blood pressure
5. Pulmonary tuberculosis
6. Neurosis
7. Venereal diseases
8. Skin diseases
9. Urine
10. Leprosy
11. Any disability
12. Stool
13. Pregnancies test
14. Other serious disease

PART B :

MEDICAL CERTIFICATE

( To be completed by a Government Medical Officer)

1. I have examined the above named student and consider that she /he is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full schooling.
2. Other comments..........................................................................................................
   ..........................................................................................................................

Date ............................................ ......................................

Signature and Official stamp

NB: (Fomu hii irudishwe kwa mkuu wa shule ikiwa imejazwa)

Fomu Na 2

## FOMU YA MAELEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANAFUNZI

**A:TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili la mwanafunzi( kama alivyo andikisha kwenye mtihani wa kidato cha nne)

..............................................................................................................................

2. Kabila.........................3.Dini............................4.Dhehebu.......................................

5. Tarehe ya kuzaliwa.................... 6. Mahali alipozaliwa .............. 7. Uraia.................

8. Shule ya sekondari alipomaliza kidato cha Nne ........................................................

**B:TAARIFA ZA MZAZI /MLEZI**

1. Jina kamili la baba .........................................................Hai/amefariki

3. Jina kamili la mama ......................................................... Hai/amefariki

Kazi ya baba.................................................................

Kazi ya mama.................................................................

4. Anwani ya baba................................................................................

Anwani ya mama

..............................................................................................................

5. Jina kamili la Mlezi..................................................................................

Kazi ya mlezi..................................................................................

Simu ..................................................................................

6. Utakuwa unakwenda wapi wakati wa likizo?.........................................

(Wakati wa likizo unatakiwa kwenda kwa mzazi au mlezi aliyetajwa tu. Kama utabadilisha mahali pa kwenda likizo, mzazi/mlezi atoe idhini kwa maandishi mwezi mmoja kabla)

7. Taja ndugu wawili (2) na wazazi /walezi wawili (2) wanaoweza kuja kukuona shuleni. Bandika picha (Passport size) zao hapa chini, na uhusiano na mawasiliano yao.

1. Jina ................. ....... ...

Uhusiano................. ......

Sehemu anayoishi.......................

Namba ya simu..........................

2. Jina............................

Uhusiano.....................

Sehemu anayoishi...........

Namba ya simu.............................................

8. Maelezo mafupi kuhusu afya ya mwnafunzi.........................................................................

9.Ninathibitisha kwamba taarifa zilizotolewa hapo juu ni kamili na sahihi.

Jina la mzazi/mlezi...........................................................................

Sahihi ya mzazi/mlezi .........................................................Tarehe ...........

**NB: (Fomu hii irudishwe kwa mkuu wa shule ikiwa imejazwa)**

**Fomu Na:3**

**MKATABA/ AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi…………………………………………………………………………… (jina kamili) ambaye ni mwanafunzi, nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa, ninakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na shule hii.

Ninaelewa wazi kwamba shuleni ni mahali pa kujifunza na mimi nina nia ya kujifunza. Ninaelewa pia kuwa nafasi hii niliyopewa ni dhamana, hivyo naahidi mbele ya wazazi/walezi wangu ya kwamba nitaitumia vema nafasi hii kwa kushirikiana na uongozi wa shule kutimiza na kutekeleza yale yote yaliyo katika maagizo haya. Nitatii na kufuata sheria za shule wakati wote. Naahidi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Naahidi pia kufanya bidii katika masomo yangu na kuwa mfano mwema kwa wenzangu wakati wote. Nafahamu kwamba kitendo che kilicho kinyume na mwenendo na taratibu za shule kinastahili adhabu kali hata kufukuzwa shule kama itakavyo amuriwa na jumuiya pamoja na baraza la ushauri la shule.

Saini ya mwanafunzi……………………………………………………………………

Tarehe……………………………………………………………

Shahidi

Jina kamili………………………………………………………………………………..

Saini…………………………………………………………………

Tarehe…………………………………………………………….

**AHADI YA MZAZI:**

Mimi……………………………………… ……………………………………………….(jina kamili) ambaye ni mzazi/mlezi

wa…………………………………………………Kidato cha……………mwaka……………………

Nimeyasoma maagizo haya na kuyaelewa vema. Nimekubali mwanangu ajiunge na shule hii. Naahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule katika kumpatia binti yangu malezi bora na nitatoa msaada kadri ya uwezo wangu nitakapotakiwa kufanya hivyo. Ninaahidi kwamba ninakubaliana na yote yaliyotajwa kwenye barua hii mfano sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule .Pia naahidi kumlipia ada na michango yote iliyoagizwa kwenye maelekezo ya kujiunga na shule hii.

Saini ya Mzazi/Mlezi…………………………………………………………………

Anuani kamili……………………………………………………………………………

Simu:…………………………………………

Tarehe:…………………………………………

**NB: (Fomu hii irudishwe kwa mkuu wa shule ikiwa imejazwa)**